

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA


(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA SIMIYU

Tel : 0282 981193

Fax : 0282 981194

Email : [dedbusega@yahoo.com](mailto:dedbusega@yahoo.com)



Sanduku la Posta 157,  
BUSEGA.

14 Machi, 2018

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega amepokea Kibali cha Ajira Mbadala kwa Watendaji wa Vijiji kwa barua ya tarehe **08 Machi, 2018** yenye **Kumb. Na. FA 170/533/01/51** kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

Kwahiyoo, anawatangazia Watanzania wote wenye Sifa na uwezo wa kujaza nafasi **09** za kazi kwa kada ya **Mtendaji wa Kijiji III** kama inavyoonekana hapa chini :-

### 1. MTENDAJI WA KIJIKI III (Nafasi 09)- TGS B

#### SIFA ZA MWOMBAJI

- Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo-Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Kuandaa Taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.

#### MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatishe nakala ya Cheti cha Kuzaliwa
3. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
4. Picha moja Passport Size iandikwe jina kwa nyuma.
5. Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (**Statement of Results havitakubalika**)
6. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma **Wasiombe Kazi** na wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.

7. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe **kwa njia ya Posta** kabla ya tarehe **28/03/2018** kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya  
S.L.P. 157  
**BUSEGA.**



Anderson N. Kabuko  
Mkurugenzi Mtendaji  
**Halmashauri ya Wilaya,**  
**BUSEGA.**